


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



Mtaa wa Sheikhbad,
S.L.P. 1004,
65101LINDI,
Barua Pepe: rbclindi@pccb.go.tz.

TANZANIA.
www.pccb.go.tz

LINDI
9 April, 2021

TAARIFA KWA UMMA

TAKUKURU MKOA WA LINDI INAMFIKISHA MAHAKAMANI WAKALA WA KUKUSANYA USHURU KWA MAKOSA YA RUSHWA PAMOJA NA KUJIPATIA FEDHA ZAIDI YA SH. MILIONI 3.2

/-

Ndugu wanahabari,

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Lindi inaendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya kuzuia na kupambana na rushwa ili kuimarisha utawala bora na kuhakikisha haki inatamalaki.

Ndugu wanahabari,

Leo tumewaita tena ili muweze kuuhabarisha umma kuwa Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Lindi kwa ushirikiano na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika mkoa huu, muda mfupi ujao tutamfikisha mahakamani mtuhumiwa kutoka wilaya ya Kilwa ambaye uchunguzi wa tuhuma dhidi yake umekamilika na kupata kibali cha kumfikisha mahakamani.

Mtuhumiwa huyo ni: Bw. Darasa Ally Mwamba, ambaye alikuwa wakala wa ukusanyaji ushuru wa Halmashauri ya wilaya ya Kilwa ambaye alijihusisha na vitendo vya rushwa pamoja na kujipatia fedha kiasi cha shilingi 3,261,000 kwa njia za udanganyifu.

Ndugu wanahabari,

Mnamo tarehe 02.01.2015 TAKUKURU Wilaya ya Kilwa ilipokea taarifa kutoka kwa msiri, kwamba kuna upotevu wa fedha za mapato ya Halmashauri.

Baada ya TAKUKURU Mkoa wa Lindi kuanza kufuatilia mapato ya Halmashauri hiyo ilibainika kuwa kuna upotevu wa fedha zinazotokana na ushuru wa kusafirisha samaki na pweza zinazotolewa na wafanyabiashara na makampuni yanayojihusisha na biashara ya usafirishaji wa samaki na pweza na fedha hizo kukusanywa na Halmashauri ya wilaya ya Kilwa na mji mdogo wa Kilwa Masoko. Baada ya kubaini upotevu wa mapato hayo ofisi iliamua kuanzisha uchunguzi wa kina kuhusu mapato hayo yanayotokana na ushuru wa samaki na pweza.

Ndugu wanahabari,

Kama ilivyo ada baada ya kupokea taarifa hizo, TAKUKURU mkoa wa LINDI ilianzisha uchunguzi mara moja kwa lengo la kubaini na kuthibitisha ukweli wa tuhuma hizo, ambapo ilibainika kuwepo kwa wizi wa fedha za makusanyo hayo ya ushuru wa samaki na pweza.

Ndugu wanahabari,

Baada ya TAKUKURU mkoa wa Lindi kukamilisha uchunguzi huu jalada hili lilipelekwa kwa mkurugenzi wa mashtaka (DPP) kwa ajili ya mapitio na kuomba kibali cha kumfikisha mahakamani mtuhumiwa aliyetajwa, na leo hii ninawajulisha kuwa kibali kimetolewa na mtuhumiwa atafikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kilwa leo hii ili kujibu mashitaka yanayomkabili ambayo baadhi yake yanaangukia katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007 pamoja na sheria nyingine kama ifuatavyo:

1. Matumizi ya nyaraka kumdanganya mwajiri.
2. Uchepushaji.
3. Matumizi mabaya ya mamlaka
4. Kughushi hesabu; pamoja na
5. Kujipatia manufaa.

Ndugu wanahabari,

TAKUKURU mkoa wa Lindi inaendelea kutoa rai kwa watumishi na wananchi wa Mkoa wa Lindi kwa ujumla kujiepusha na vitendo vyovyote vya Rushwa kwani kila mmoja wetu anajua madhara yatokanayo na vitendo vya Rushwa, na kamwe TAKUKURU kwa kutumia mamlaka tuli~~y~~opewa kwa mujibu wa sheria hatuta sita kuendelea kuwachukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani wale wote ambao wanajihusisha na vitendo vya Rushwa.

Pia nichukue nafasi hii kutoa rai kwa watumishi wote wa serikali na sekta binafsi katika mkoa wa Lindi, kuwa Taifa letu linahitaji maendeleo, hivyo kila mmoja wetu anatakiwa kuendelea kuzingatia viapo vya utumishi na maadili ya kazi zake, pamoja na kufahamu kuwa Rushwa haijawahi kukubalika mahali popote na katika jamii yoyote ile.

Ndugu wanahabari,

TAKUKURU Mkoa wa Lindi inaendelea kuwashukuru wananchi, vyombo vya Habari, pamoja na taasisi mbalimbali (binafsi na za serikali) katika Mkoa wa Lindi kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kuutoa kwa ofisi zetu ikiwepo kutoa taarifa mbalimbali za vitendo vya rushwa. Aidha, tunawaomba wananchi na wadau wote waendeleo kutuunga mkono kwa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa kutumia njia mbalimbali hususani kupitia simu yetu ya bure ya namba ya dharura **113** kwani mapambano dhidi ya rushwa si ya TAKUKURU peke yake bali ni ya jamii nzima kwa ujumla.

Imetolewa na:

Eng. Abnery J. Mganga
Mkuu wa TAKUKURU (M) Lindi